Mwongozo wa Mabadiliko ya Medicaid

Taarifa kwa kitengo cha huduma kwa wateja na watoaji huduma:

Mswada ufuatao wa maongezi ya simu na maswali yanayoulizwa mara kwa mara yalibuniwa ili kusaidia wanachama wa Medicaid kufahamu wanachofaa kufanya baada ya mpango wao wa bima kupitiwa**.** Tunapendekeza kwamba ujaribu kutumia taarifa changamano zilizo katika sehemu za mswada na maswali yanayoulizwa mara kwa mara, mara nyingi iwezekanavyo unapozungumzia mabadiliko haya.

Mabadiliko katika Medicaid na hatua ambazo mtu anafaa kuchukua ni ngumu sana kuelezea na kuelewa. Tungependa kuifanya shughuli hii iwe rahisi zaidi iwezekanavyo kwako wewe **na** kwa watu unaohudumia. Taarifa changamano zilizo katika hati hii zimepitia mchakato kabambe wa mapitio wa kuepesisha lugha ili kusaidia kufanya taarifa hizi muhimu ziwe rahisi kuelewa na kutumia.

Mswada:

Wakati wa janga la COVID-19, watu waliokuwa na Medicaid waliendelea kuwa na bima hiyo, hata ikiwa hawakuwa wanastaki kupata bima hiyo tena. Ugonjwa wa COVID-19 hauchukuliwi tena kama hatari kubwa kwa afya ya umma. Hii inamaanisha kwamba tunahitaji kupitia mipango yote ya bima ya Medicaid ili kubaini ni nani ambaye bado anastahiki kupata bima hii.

Idara ya Huduma za Wafanyakazi (DWS) ilianza kufanya mapitio ya ustahiki wa Medicaid mnamo Machi 1, 2023. **Hii inamaanisha kwamba wewe au jamaa yako anaweza kupoteza bima yake ya Medicaid ikiwa hastahiki kupata Medicaid tena.** Tutapitia mpango wako wa bima kabla ya Machi 2024 ili kubaini ikiwa bado unastahiki kupata Medicaid.

Utapokea mawasiliano kwa njia ya barua ya posta au barua pepe wakati mpango wako wa bima utakuwa tayari kupitiwa. Unaweza kupiga simu kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi au utembelee myCase ikiwa ungependa kujua mpango wako wa bima utapitiwa mwezi gani.

Huhitaji kufanya chochote hadi wakati mpango wako wa bima utapitiwa. Unaweza kutumia bima yako kama kawaida hadi tutakapokamilisha kupitia mpango wako wa bima. Unachohitaji kufanya tu ni kuhakikisha kwamba taarifa zako tulizo nazo ni sahihi.

- **Hakikisha kwamba taarifa zako zimesasishwa.**

- Unaweza kuangalia ili kuhakikisha kwamba taarifa zako ni sahihi katika akaunti yako ya myCase.

Utahitaji kusasisha taarifa zako ikiwa umehama hivi karibuni au ikiwa maelezo yako yoyote ya mawasiliano yamebadilika (kama nambari ya simu au anwani ya barua pepe). Idara ya Huduma za Wafanyakazi (DWS) itakutumia barua itakayosema jambo **moja** kati ya yafuatayo:

- Bado **unastahiki** kupata bima ya afya ya Medicaid.
- **Hustahiki** kupata Medicaid tena. Barua hiyo itakuwa na hatua ambazo unaweza kuchukua ili kupata bima tofauti ya afya.
- Wanahitaji **taarifa zaidi** ili kubaini ikiwa bado unastahiki kupata Medicaid. Barua hiyo itakuwa na fomu unazofaa kujaza na huenda ikakuomba hati za kuunga mkono ombi lako (kama vile hati za malipo ya mshahara, taarifa za benki, n.k.).

Zingatia tarehe za mwisho zilizowekwa.

Unaweza kupoteza bima yako ya Medicaid ukikosa kurejesha fomu au ukipitisha tarehe za mwisho zilizowekwa.

Je, ungependa niangalie ili kuhakikisha kwamba taarifa zako zimesasishwa?
Ninaweza kukusasishia taarifa hizo sasa hivi ukipenda, au unaweza kupiga simu kwa huduma yoyote kati ya zifuatazo ili kusasisha taarifa zako:

- Bima yako ya afya
- Idara ya Huduma za Wafanyakazi kupitia 1-866-435-7414
- Mtumishi wa huduma kwa wateja wa bima ya afya kupitia 1-866-608-9422

Je, una maswali yoyote?

Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Je, kwa nini kuna mabadiliko katika Medicaid?

Wakati wa janga la COVID-19, watu waliokuwa na Medicaid waliendelea kuwa na bima hiyo, hata ikiwa hawakuwa wanastaki kupata bima hiyo tena. Ugonjwa wa COVID-19 hauchukuliwi tena kama hatari kubwa kwa afya ya umma. Hii inamaanisha kwamba tunahitaji kupitia mipango yote ya bima ya Medicaid ili kubaini ni nani ambaye bado anastahiki kupata bima hii.

Idara ya Huduma za Wafanyakazi (DWS) ilianza kufanya mapitio ya ustahiki wa Medicaid mnamo Machi 1, 2023. **Hii inamaanisha kwamba wewe au jamaa yako anaweza kupoteza bima yake ya Medicaid ikiwa hastahiki kupata Medicaid tena.** Tutapitia mpango wako wa bima kabla ya Machi 2024 ili kubaini ikiwa bado unastahiki kupata Medicaid.

Je, ninahitaji kufanya nini?

Huhitaji kufanya chochote hadi wakati mpango wako wa bima utapitiwa. Unaweza kutumia bima yako kama kawaida hadi tutakapokamilisha kupitia mpango wako wa bima. Hakikisha kwamba taarifa zako za mawasiliano tulizo nazo ni sahihi. Unaweza kuangalia ili kuhakikisha kwamba taarifa zako zimesasishwa katika akaunti yako ya myCase.

- Sasisha taarifa zako ikiwa umehama hivi karibuni au ikiwa maelezo yako yoyote ya mawasiliano yamebadilika (kama nambari ya simu au anwani ya barua pepe).

Pia unaweza kupiga simu kwa huduma yoyote kati ya zifuatazo ili kusasisha taarifa zako.

- Bima yako ya afya
- Idara ya Huduma za Wafanyakazi kupitia 1-866-435-7414
- Mtumishi wa huduma kwa wateja wa bima ya afya kupitia 1-866-608-9422

Je, nitajua vipi ikiwa bado ninastahiki kupata Medicaid?

Angalia barua za posta, barua pepe na akaunti yako ya myCase kwa umakini. Idara ya Huduma za Wafanyakazi (DWS) itasasisha akaunti yako ya myCase na kukutumia barua ya posta au barua pepe baada ya kupitia mpango wako wa bima.

Idara ya Huduma za Wafanyakazi itakutumia barua itakayosema jambo **moja** kati ya yafuatayo:

- **Bado unastahiki** kupata bima ya afya ya Medicaid.
- **Hustahiki** kupata Medicaid tena. Barua hiyo itakuwa na hatua ambazo unaweza kuchukua ili kupata bima tofauti ya afya.
- Wanahitaji **taarifa zaidi** ili kubaini ikiwa bado unastahiki kupata Medicaid. Barua hiyo itakuwa na fomu unazofaa kujaza na huenda ikakuomba hati za kuunga mkono ombi lako (kama vile hati za malipo ya mshahara, taarifa za benki, n.k.).

Je, nitafahamu vipi tarehe ya kupitiwa kwa mpango wangu wa bima?

Unaweza kuangalia akaunti yako ya myCase au kupiga simu kwa huduma yoyote kati ya zifuatazo ikiwa ungependa kujua mpango wako wa afya utapitiwa mwezi gani:

- Bima yako ya afya
- Idara ya Huduma za Wafanyakazi kupitia 1-866-435-7414
- Mtumishi wa huduma kwa wateja wa bima ya afya kupitia 1-866-608-9422

Je, ninahitaji kufanya nini baada ya ombi langu kupitiwa?

Fuata maagizo yaliyo kwenye barua utakayopokea kutoka kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi. Jaza fomu **zote** za mapitio na uzitume kwa njia ya posta au barua pepe kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi haraka iwezekanavyo ili kuepuka kukosa bima ya afya wakati wowote.

Huenda wakahitaji taarifa zaidi ili kubaini ikiwa bado unastahiki kupata Medicaid. Watakutumia barua itakayokuwa na fomu unazofaa kujaza na huenda ikakuomba hati za kuunga mkono ombi lako (kama vile hati za malipo ya mshahara, taarifa za benki, n.k.) ikiwa watakutumia barua. Jaza na utume fomu hizo haraka iwezekanavyo ili kuepuka kukosa bima ya afya wakati wowote.

Tuma fomu zako za mapitio zilizokamilishwa kwa:

DWS, PO Box 143245, Salt lake City, UT 84114-3245

Je, ni nini kitatokea ikiwa sitatuma fomu hizo au hati za kuunga mkono ombi langu?

Huenda ukapoteza bima yako ya afya. Tuma fomu au hati zozote za kuunga mkono ombi lako kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi haraka iwezekanavyo. Una **siku 90** za kuwaomba wapitie mpango wako tena ikiwa utapoteza bima yako ya Medicaid kwa kukosa kutuma fomu au hati za kuunga mkono ombi lako.

Tuma fomu zako za mapitio zilizokamilishwa kwa:

DWS, PO Box 143245, Salt lake City, UT 84114-3245)

Je, ninaweza kufanya nini ikiwa nitapoteza bima yangu ya afya ya Medicaid?

Tungependa wakazi wote wa Utah wapate bima ya afya na wawe na bima kila wakati. Utapokea yafuatayo ikiwa hustahiki kupata Medicaid tena:

- Barua itakayokufahamisha kuhusu wakati ambapo bima yako ya afya ya Medicaid itaacha kutumika.
- Utahamishwa kiotomatiki hadi katika Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa (ikiwa tu kama utawasilisha fomu na hati za kuunga mkono ombi lako zinazohitajika).
- Taarifa kuhusu Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa.
- Taarifa kuhusu jinsi ya kukata rufaa. Hii ina maana kwamba unaweza kuwaomba wapitie mpango wako wa bima tena ikiwa unadhani kwamba unafaa kustahiki, lakini Idara ya Huduma za Wafanyakazi ilikutumia barua inayosema kwamba hustahiki kupata Medicaid tena.

Zingatia tarehe za mwisho zilizowekwa.

- Sharti uwasilishe rufaa ndani ya siku 90.
- **Hutahamishwa** kiotomatiki na kuwekwa chini ya Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa ikiwa utapoteza bima yako ya Medicaid kwa kukosa kuwasilisha fomu na hati za kuunga mkono ombi lako ulizoombwa.

Maana ya kuhamishwa kiotomatiki na kuwekwa chini ya huduma ya bima ya afya ya serikali ya taifa ni nini?

Watu wasiostahiki kupata Medicaid tena watahamishwa kiotomatiki na kuwekwa chini ya Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa (healthcare.gov). Hivi sasa kuna mchakato otomatiki wa kumhamisha mtu ilmradi tu itabainishwa kwamba anastahiki. Huwezi kuhamishwa ikiwa utapoteza bima ya Medicaid kwa kukosa kukamilisha au kurejesha fomu zako.

Kuna machaguo gani mengine ya bima ya afya?

Watu wasiostahiki kupata bima ya afya ya Medicaid bado wanaweza kupata bima kupitia Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa au healthcare.gov. Watu wengi wanastahiki kuweza kuweka pesa za akiba katika bima ya afya ili kupunguza malipo ya bima ya kila mwezi na kiasi cha pesa wanachohitajika kujilipia kila wanapotafuta matibabu. Pesa za akiba hulingana na ukubwa wa kaya na mapato ya mtu huyo. Bima zote za afya za serikali ya taifa hulipia dawa zilizoagizwa na daktari, wakati wa kutembelea daktari, matatizo ya afya yanayohitaji matibabu ya haraka, wakati wa kutembelea hospitali, na zaidi.

Watu wanaopoteza bima ya Medicaid wana hadi siku 60 za kuomba kupata bima ya afya katika Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa. Bima za afya kwa kawaida huwa na kipindi cha kujisajili kila mwaka ambapo watu wanaweza kujiandikisha kupata bima ya afya. Watu huruhusiwa tu kujiandikisha ndani ya kipindi hicho isipokuwa kama mtu ana kisa cha kipekee kinachomruhusu kuandikishwa nje ya kipindi hicho. Ikiwa mtu hastahiki kupata Medicaid tena, inachukuliwa kwamba ana kisa cha kipekee kinachomruhusu kuandikishwa nje ya kipindi kilichowekwa. Hii inamaanisha kwamba watu huwa na **siku 60 baada ya kupoteza bima yao ya Medicaid** ili waweze kujiandikisha kupata bima mpya ya afya.

Utahitaji kusubiria hadi kipindi kitakachofuata cha kujiandikisha ikiwa hutajisajili kupata bima mpya ya afya ndani ya siku 60 baada ya kufungwa kwa bima yako ya Medicaid. Pia ni muhimu kufahamu kwamba **hutahamishwa** kiotomatiki na kuwekwa chini ya huduma ya bima ya afya ya serikali ya taifa ikiwa utapoteza bima yako ya Medicaid kwa kutozingatia tarehe za mwisho zilizowekwa au kwa kukosa kuwasilisha fomu na hati za kuunga mkono ombi lako.

Mfano wa kisa cha kipekee kinachomruhusu mtu kuandikishwa nje ya kipindi kilichowekwa ni gani?

- Ikiwa utafunga ndoa au kupata talaka.
- Ikiwa utapata au kuasili mtoto.
- Ikiwa mtu anayeishi nyumbani kwako atafariki (mtu unayejaza kama mtegemezi wako unapokamilisha fomu za marejesho ya kodi).
- Mabadiliko ya ukubwa wa kaya (idadi ya watu unaojaza kama wategemezi wako unapokamilisha fomu za marejesho ya kodi).
- Ikiwa mapato ya kaya yako yatabadilika (kuongezeka au kupungua).
- Ikiwa hustahiki tena kupata Medicaid au bima ya CHIP kwa kuwa mapato yako yameongezeka.
- Ukipoteza bima ya afya uliyopata kupitia mwajiri au kazi yako.
- Ikiwa mpango wako wa bima ya afya utabatilisha bima yako, hata ikiwa umelipia bima yako.
- Ikiwa muda wa kutumika kwa bima yako ya COBRA utaisha.
- Ukifikisha miaka 26 na huwezi kuendelea kuwa chini ya bima ya afya ya mzazi wako tena.
- Utahamia katika mji, jimbo, au msimbo tofauti wa eneo.
- Utatoka katika jela au gereza.
- Utakuwa mwathiriwa wa ghasia za nyumbani.
- Ikiwa hitilafu fulani itakuzuia kupata bima ya afya baada ya kuruhusiwa kuacha kuhudumu katika Jeshi.

Piga simu kwa 211 ili kupanga miadi isiyo na malipo na Take Care Utah ikiwa unahitaji msaada wa kujiandikisha kupata bima mpya ya afya.

Je, bima yangu mpya ya afya itakuwa na gharama ya juu?

Watu wengi hustahiki kuweza kuweka pesa za akiba katika bima ya afya ili kupunguza malipo ya bima ya kila mwezi na kiasi cha pesa wanachohitajika kujilipia kila wanapotafuta matibabu. Pesa za akiba hulingana na ukubwa wa kaya na mapato yako. Bima zote za afya za serikali ya taifa hulipia dawa zilizoagizwa na daktari, wakati wa kutembelea daktari, matatizo ya afya yanayohitaji matibabu ya haraka, wakati wa kutembelea hospitali, na zaidi.

Je, ninafaa kuwasilisha rufaa vipi?

Maana ya kukata rufaa ni kuomba Idara ya Huduma za Wafanyakazi ipitie mpango wako wa bima tena ikiwa unadhani kwamba unafaa kustahiki, lakini walikutumia barua inayosema kwamba hustahiki kupata Medicaid tena. Ikiwa hukubaliani na uamuzi wa ustahiki na ungependa kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo, sharti utume ombi la kusikizwa kwa rufaa yako ndani ya muda wa siku 90 tangu tarehe ya kuandikwa kwa taarifa usiyokubaliana nayo.

Maombi ya kusikizwa kwa rufaa za ustahiki wa Medicaid na CHIP yanafaa kuwasilishwa kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi (DWS), Kitengo cha Kufanya Maamuzi. Utahitaji kukamilisha fomu hiyo na kuirejesha kwa DWS. Tembelea tovuti ya DWS ili kupata fomu hiyo na taarifa zaidi kuhusu kukata rufaa. Ikiwa una maswali, unaweza kutuma barua pepe kwa fairhearings@utah.gov au kupiga simu kwa 1-877-837-3247.

Tuma fomu yako iliyokamilishwa ya kuomba rufaa kwa:
Department of Workforce Services – Fair Hearings
PO Box 143245, Salt Lake City, UT 84114-3245

Je, ninaweza kukamilisha mapema kupitiwa kwa bima yangu ya Medicaid?

Hapana. Tunakuomba usubirie hadi mpango wako wa bima utakaporatibiwa kufanyiwa mapitio kwa sababu tuna mipango mingi ya bima ya kupitia. Huhitaji kufanya chochote hadi wakati mpango wako wa bima utapitiwa. Unaweza kutumia bima yako kama kawaida hadi tutakapokamilisha kupitia mpango wako wa bima.

- Hakikisha kwamba taarifa zako za mawasiliano tulizo nazo ni sahihi. Unaweza kuangalia ili kuhakikisha kwamba taarifa zako zimesasishwa katika akaunti yako ya myCase.
- Sasisha taarifa zako ikiwa umehama hivi karibuni au ikiwa maelezo yako yoyote ya mawasiliano yamebadilika (kama nambari ya simu au anwani ya barua pepe).

Je, nitafanyaje ili mpango wangu wa bima upitiwe kwa haraka?

Huhitaji kufanya chochote hadi wakati mpango wako wa bima utapitiwa. Unaweza kutumia bima yako kama kawaida hadi tutakapokamilisha kupitia mpango wako wa bima. Hata hivyo, kuna mambo machache unayoweza kufanya ili kufanya mchakato huo uende haraka na kwa urahisi:

- Sasisha taarifa zako ikiwa umehama hivi karibuni au ikiwa maelezo yako yoyote ya mawasiliano yamebadilika (kama nambari ya simu au anwani ya barua pepe). Unaweza kusasisha taarifa zako katika akaunti yako ya myCase.
- Idara ya Huduma za Wafanyakazi itakujulisha ikiwa wanahitaji hati zozote za kuunga mkono ombi lako ili kubaini kama bado unastahiki kupata Medicaid (kama hati za malipo ya mshahara, taarifa za benki, n.k.). **Tuma hati hizi haraka iwezekanavyo.** Hii itasaidia wahudumu wanaobaini ustahiki wakamilishe kupitia mpango wako wa bima haraka zaidi.

Je, nifanye nini ikiwa siishi Utah tena?

Bima ya Medicaid ya Utah ni ya watu wanaoishi katika jimbo la Utah tu. **Sharti** upige simu kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi na uwajulishe kwamba umehamia jimbo lingine.

Je, nitafunga vipi mpango wangu wa bima ya Medicaid?

Piga simu kwa Idara ya Huduma za Wafanyakazi kupitia 1-866-435-7414 kisha uwaombe wafunge mpango wako wa bima.

Nitamsaidia vipi mtu ambaye amepoteza bima yake ya afya ya Medicaid?

Hakikisha kwamba taarifa za mtu huyo zimesasishwa.

Anaweza kuangalia mtandaoni ili kuhakikishwa kwamba taarifa zake ni sahihi kwenye akaunti yake ya myCase kwa kutembelea jobs.utah.gov/mycase au kupiga simu kwa huduma zozote zifuatazo ili kusasisha taarifa zake.

- Bima yake ya afya
- Idara ya Huduma za Wafanyakazi kupitia 1-866-435-7414
- Mtumishi wa huduma kwa wateja wa bima ya afya kupitia 1-866-608-9422

Mwambie mtu huyo aangalie akaunti yake ya myCase, barua za posta, na barua pepe kwa umakini.

Idara ya DWS itasasisha akaunti yake ya myCase na kumtumia barua ya posta au barua pepe baada ya kupitiwa kwa mpango wake wa bima. Barua hiyo itasema jambo **moja** kati ya yafuatayo:

- Bado **anastahiki** kupata bima ya afya ya Medicaid.
- Mtu huyo **hastahiki** kupata Medicaid tena. Barua hiyo itakuwa na hatua ambazo anaweza kuchukua ili kupata bima tofauti ya afya.
- **Taarifa zaidi zinahitajika** ili kubaini ikiwa bado anastahiki kupata Medicaid. Barua hiyo itakuwa na fomu anazofaa kujaza na huenda ikamuomba hati za kuunga mkono ombi lake (kama vile hati za malipo ya mshahara, taarifa za benki, n.k.). **Anahitaji kutuma hati hizo haraka iwezekanavyo ili asipitishe tarehe ya mwisho iliyowekwa.**

Hakikisha kwamba mtu huyo anafahamu kuwa ana **siku 90** tu za kuomba Idara ya Huduma za Wafanyakazi ipitie mpango wake wa bima tena ikiwa amepoteza bima yake ya Medicaid kwa kukosa kuwasilisha fomu na hati za kuunga mkono ombi lake. Pia ni muhimu kumfahamisha mtu huyo kwamba **hatahamishwa** kiotomatiki na kuwekwa chini ya Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa ikiwa atapoteza bima yake ya Medicaid kwa

kutozingatia tarehe za mwisho zilizowekwa au kwa kukosa kuwasilisha fomu na hati za kuunga mkono ombi lake.

Msaidie mtu huyo kujiandikisha kupata bima tofauti ya afya.

Watu wanaopoteza bima yao ya Medicaid kwa sababu hawakuwasilisha hati zao, huenda bado wana siku 90 za kuomba kupata bima tena. Mwambie arejeshe fomu ya mapitio au hati nyingine inayohitajika na idara ya DWS mara moja,

Watu wasiostahiki kupata bima ya afya ya Medicaid bado wanaweza kupata bima kupitia **Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa au healthcare.gov**. Watu wengi wanastahiki kuweza kuweka pesa za akiba katika bima ya afya ili kupunguza malipo ya bima ya kila mwezi na kiasi cha pesa wanachohitajika kujilipia kila wanapotafuta matibabu. Pesa za akiba hulingana na ukubwa wa kaya na mapato ya mtu huyo. Bima zote za afya za serikali ya taifa hulipia dawa zilizoagizwa na daktari, wakati wa kutembelea daktari, matatizo ya afya yanayohitaji matibabu ya haraka, wakati wa kutembelea hospitali, na zaidi.

Watu wanaopoteza bima ya Medicaid wana hadi siku 60 za kuomba kupata bima ya afya katika Huduma ya Bima ya Afya ya serikali ya taifa. Bima za afya kwa kawaida huwa na kipindi cha kujisajili kila mwaka ambapo watu wanaweza kujiandikisha kupata bima ya afya. Watu huruhusiwa tu kujiandikisha ndani ya kipindi hicho isipokuwa kama mtu ana kisa cha kipekee kinachomruhusu kuandikishwa nje ya kipindi hicho. Ikiwa mtu hastahiki kupata Medicaid tena, inachukuliwa kwamba ana kisa cha kipekee kinachomruhusu kuandikishwa nje ya kipindi kilichowekwa. Hii inamaanisha kwamba watu huwa na **siku 60 baada ya kupoteza bima yao ya Medicaid** ili waweze kujiandikisha kupata bima mpya ya afya.

Tembelea healthcare.gov/medicaid-chip/transfer-to-marketplace/ ili kupata maelezo zaidi.